SHULE YA UPILI YA GATITU S.L.P 01030 ,327 GATUNDU

MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA KWANZA
KIDATO CHA TATU-2016

(muda-saa $2^{3}/_{4}$)

jina:.....darasa.....nambari.....

A) UFAHAMU *(alama 15)*

Soma Makala Yafuatayo Kisha Ujibu Maswali.

Ni dhahiri shahiri kwamba uharamia umechipuka kama desturi na mfumo wa maisha katika siku za hivi karibuni. Janga hili limeshamiri hususan pembeni mwa bara la Afrika na kanda ya Afrika mashariki. Taarifa za uharamia zimetawala vyombo vya habari kiasi cha kwamba haipiti siku bila kuripotiwa visa vipya vya matendo haya mabovu ambayo yanaweza tu kumithilishwa na uhayawani. Matukio haya yamewalimbikizia mabaharia na nchi husika, simanzi na masaibu yasiyoweza kutiwa kwenye mizani.

Yamkini tatizo hili halitokei pasi na kumotishwa na kitita cha fidia kinachodaiwa na maharamia hawa. Aghalabu, suala hili lahusishwa pakubwa na azma na ari ya kuendeleza ujambazi wa kimataifa sawia na ulipuaji wa bomu mijini Nairobi na Dar-es-Salaam mnamo Agosti 7, 1998, na tukio la Septemba 11, mwaka wa 2001 kule marekani. Maafa na uharibifu wa mali si hoja, la mno kwa maharamia ni kutosheleza matakwa yao. Kwa upande mwingine, ukosefu wa tawala-wajibika katika maeneo kunakotokea unyama huu ni thibitisho tosha la mazingara yanayowezesha na kuruhusu kuchipuka kwa janga hili.

Mchipuko wa baa la uharamia umelengwa jamii ya kimataifa ambayo ni mhudumu mkuu wa harakati za kusitisha majanga makubwa kama vile njaa, umaskini na magonjwa yaliyosheheni pakubwa barani. Bila shaka, hili ni suala linalosawisishwa na 'kinyume mbele.' Maharamia wanatishia utangamano wa kimataifa wanapotibua usafiri wa abiria na shehena zinazoelekezwa sehemu tofauti ulimwenguni.

Matumizi ya kidiplomasia na mashauriano hayaelekei kuzalisha matunda katika juhudi za kudhibiti uharamia. Zaidi ya hayo, matumizi ya nguvu yahusishayo mashambulizi pamoja na maharamia kufunguliwa mashtaka nchini Kenya na Ufaransa kunaelekea kuzipiga jeki juhudi za uharamia ulimwenguni. Aidha, utawala wa nchi kunakochipuka uharamia haujajizatiti kuharamisha doa hili linalotisha ustawi wa kimataifa.

Mathalan, ni jambo lisilopingika inapobainika kuwa uharamia umedumaza biashara ya kimataifa, hali inayochangia upungufu na ucheleweshaji wa bidhaa muhimu zinazoendeleza ustawi wa uchumi. Dosari hii inaelekea kukwamiza mojawapo wa malengo ya maendeleo ya milenia yanayosisitiza uimarishaji na ushirikiano wa maendelo na upanuzi wa masoko ulimwenguni. Harakati za kitalii katika kanda ya mashariki ya bara

la Afrika zimehujumiwa. Ni muhali kwa utalii kustawi kwenye maeneo yaliyo na tishio la usalama. Itakumbukwa bayana kwamba watalii hawasafiri tu kwa ndege bali hata kwa meli.

Jitihada za kuweka laini za mawasiliano chini ya bahari ili kurahisisha na kupunguza gharama za mtandao ulimwenguni ni ndoto ambayo haijatimia hadi hivi sasa, kufuatia juhudi za maharamia katika bahari ya Hindi. Kwa mujibu wa hali hii, mawasiliano mepesi na nafuu yasitarajiwe hivi karibuni. Licha ya hayo, shughuli za uvuvi na biashara nyinginezo kwenye kanda ya mwambao zimetiliwa shaka si haba.

Itabidi mikakati na suluhisho la kudumu liweze kupatikana na vitendo vya uharamia viweze kusitishwa

Maswali

(a) Kwa nini uharamia umetamalaki ulimwenguni? (alama3)

.....

.....

.....

(b) Fafanua dhana ya kinyume–mbele kwa mujibu wa taarifa hii.(alama2)

.....

.....

(c) Uharamia unaelekea kumtia hofu mwandishi. Fafanua. (alama3)

.....

.....

.....

.....

(d) Thibitisha kuwa Kenya imeathirika pakubwa kutokana na vitendo vya uharamia (alama4)

.....

.....

.....

.....

(e) Ukirejelea kifungu, eleza maana ya:- (alama 3)

(i)Uharamia.....

ii)Mtandao.....

iii)Mwambao.....

B) *MATUMIZI YA LUGHA* ***(alama 35)***

a) Tofautisha kati ya sauti ghuna na sauti sighuna/hafifu (alama2)

.....

.....

b) Ainisha

Kilichopikika (alama 3)

.....

.....

.....

c)Tunga sentensi kudhihirisha matumizi ya ngeli ya (alama 2)

i)U-ZI

.....

ii)I-ZI

.....

d)Onyesha matumizi ya kwa katika sentensi hizi (alama 3)

i)Tulifanya kazi kwa bidii

.....

ii)Nyaga alikwenda hospitalini kwa matibabu

.....

iii)Sakaja alikula ugali kwa mkono

.....

e)Tunga sentensi moja katika wakati uliopita hali ya kuendelea (alama2)

.....

f)Yakinisha sentensi ifuatayo (alama 2)

Hatujakubaliana tuachane na tofauti zetu za kifamilia.

.....

g)Taja maneno mawili yenye muundo wa silabi funge. (alama1)

.....

h)Tunga sentensi kudhihirisha matumizi ya *nukta pacha* (alama 2)

.....

i)Andika sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa (alama 3)

Fatuma alisema "Sofia alinileta nguo ambayo nitavaa kesho"

.....

.....

j)Unda nomino kutokana na nomino hizi (alama 2)

i) Mvuvi.....

ii)Uchaguzi.....

k)Andika kinyume cha sentensi ifuatayo (alama 2)

Mama alimeza dawa yote na kumshukuru dada

.....

l)Tofautisha sentensi zifuatazo kimaana (alama 2)

i) Mutua amekula mkate wote

.....

ii) Mutua amekula mkate wowote

.....

m) Bainisha vielezi na ueleze ni vya namna gani katika sentensi hii. (alama 2)

i.Sipendi wanaohama hivi hivi ili kuenda kuishi kizungu.

.....

ii.Wariaula alidungwa sindano akalala fo fo fo.

.....

n) Tumia kiwakilishi cha *-a* unganifu kutunga sentensi katika ngeli ya KU - KU. (alama 1)

.....

o) Geuza sentensi uliyopewa iwe katika hali ya udogo. (alama 2)

Nyumba yenyewe ilijengwa karibu na mto unaofurika mara kwa mara.

.....

p) Tumia neno 'mle' kwenye sentensi kama: (alama 4)

i. Kivumishi .....

ii. Kitenzi.....

iii. Kiwakilishi .....

iv. Kielezi .....

C) *SHAIRI* *(alama 20)*

SOMA SHAIRI LIFUATALO KISHA UJIBU MASWALI

Msambe naja kuteta, nina wema wa kalima,
Moyo wanikatakata, maini yangu yachoma,
Ili nipate takata, ukweli wote 'tasema,
Anayekataa pema, pabaya panamuita.

Muacha pema hujuta, aendapo si salama,
Bahati ni kama nyota, humemeta na kuzima,
Sikimbilie mafuta, ukatae kula sima,
Anayekataa pema, pabaya panamuita.

Haraka zina matata, angaza mbele na nyuma,
Tenda mambo kwa kusita, usije ukalalama,
Keti pako ukipata, kwa muradi wa uzima,
Anayekataa pema, pabaya panamuita.

Pema si penye mafuta, au pa wali na nyama,
Pema watu hutafuta, utulivu na hekima,
Si hoja penye ukata, pa watu hali ya nyuma,
Anayekataa pema, pabaya panamuita.

Mahali pema ambata, kwa vitendo na huduma,
Sikae penye matata, palipojaa hasama,
Lau kama pamemeta, hapafai kwa daima,
Anayekataa pema, pabaya panamuita.

Maswali

(a) Lipe anwani mwafaka shairi hili. (alama 1)

.....

(b) Bainisha bahari mbili za shairi hili. (alama 2)

.....

.....

(c) Eleza muundo wa shairi hili. (alama 4)

.....

.....

.....

.....

.....

(d) Fafanua dhamira ya mshairi. (alama 1)

.....

.....

(e) Andika ubeti wa tatu kwa lugha ya nathari. (alama 4)

.....

.....

.....

.....

(f) Onyesha jinsi mshairi alivyoutumia uhuru wake. (alama 3)

.....

.....

.....

(g) Kwa kutoa mifano, bainisha tamathali ***mbili*** za usemi zilizotumika katika shairi.

(alama 2)

.....

.....

(h) Eleza maana ya msamiati ufuatao. (alama 3)

(i) Kalima:.....

(ii) Mafuta:.....

(iii) Ukata:.....

D) ***ISIMU- JAMII*** ***(alama 10)***

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata.

"Ndugu na madada, sote tumealikwa katika karamu hii ya Bwana kabla ya kujongea mezani pake, Bwana. Pana haja ya kutakasa nyoyo zetu na kujutia madhambi yetu. Sisi sote ni watenda dhambi na inastahili kumwendea ili aweze kutuondolea madhambi yetu."

Maswali

(i) Weka maneno haya katika sajili yake. (alama 2)

.....

(ii) Eleza sifa za matumizi lugha katika sajili hii. (alama 8)

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

E) FASIHI:KIDAGAA KIMEMWOZEA na Ken Walibora (alama 20)

jibu swali la kwanza AU la pili- usijibu maswali yote mawili

1.'Alaa ! Mtoto mdogo hata ubwabwa haujakutoka shingoni unakimbilia nini..... ?'

a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)

b) Bainisha tamathali mbili za usemi katika dondoo. (alama 2)

c) Kwa kutoa mifano mitatu, onyesha kwamba kwa hakika ubwabwa ulikuwa umemtoka shingoni anayerejelewa (alama 6)

d) Asasi inayorejelewa katika muktadha huu inakumbwa na matatizo mengi. Kwa kurejelea riwaya nzima, jadili matatizo yoyote manne kwa mifano mwafaka (alama

2 "Amani ni mhusika anayestahili kuigwa katika jamii." Thibitisha ukweli wa kauli hii ukirejelea Riwaya ya Kidagaa Kimemwozea. (alama 20)

********** ******* Heri Njema**********